# Pwani Leo

Toleo la Januari 2023|Kazi iendelee

*Imetolewa na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Pwani*

## RC kunenge; azitaka Halmashauri na Taasisi za Serikali kuhakikisha zinaongeza mapato ili kuinua uchumi wa Mkoa...uk2



## Pwani Kuendela Kufungua Mtandao wa miundombinu ya Barabara...





Mkuu wa mkoa wa Pwani Mhe.Abubakar Kunenge akihutubia katika kikao cha ushauri cha mkoa wa pwani kilichofanyika tarehe 5.1.2023.Picha na ayubu simba.

## Ras Pwani alikabidhi Jukwaa la Uwezeshaji Wananawake kiuchumi kampuni ya Go MAMA yenye mtaji na hisa Bilioni 50

## TASAF yatoa Vifaa vya Usafi kwa Watoto wa Kike Pwani...



# Pwani Leo

Toleo la Januari 2023|Kazi iendelee

*Imetolewa na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Pwani*

MKuuwa mkoa wa Pwani,alhaj Abubakari Kunenge amezitaka Halmashauri na Taasisi za Serikali kuhakikisha zinaongeza mapato pamoja na kuibua vyanzo vipya vya mapato ili kuinua uchumi wa Mkoa.

Aidha ameyataka mabaraza ya madiwani kuzungumza uchumi na  fursa zilizopo ili kwenda na kipaombele cha kuinua uchumi.

Akizungumza katika kikao Cha Ushauri Cha mkoa (RCC) Januari 5,2023 Kunenge alieleza ,wote kwa umoja wazungumzie mapato ili kupunguza kukopa, kwani mkoa huo ni wa viwanda haiwezekani kuona unashuka kiuchumi.

“Halmashauri ziongeze mapato, tuende pamojaa na uwezo wa kiuchumi, na niseme hapo nikizungumzia mapato sio halmashauri tuu na Taasisi zetu za Serikali zihakikishe zinaongeza mapato,hata Kama mnakusanya ,mtuambie mnakisanya kiasi gani na malengo yenu ni yapi”alifafanua Kunenge.



Mkuu wa Mkoa wa Pwani Mhe.Abubakar Kunenge akihutubia kikao cha ushauri cha mkoa. Picha na Ayubu Simba.



# Pwani Leo

Toleo la Januari 2023|Kazi iendelee

*Imetolewa na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Pwani*




Naibu Waziri wa Ardhi Mhe.Ridhiwani Kikwete Mbunge wa Jimbo la Chalinze akichangia katika kikao cha Ushauri mkoa wa Pwani .Picha na Ayubu Simba



Mhe.Michael Mwakamo Mbunge wa Jimbo la Kibaha vijijini  akichangia katika kikao cha Ushauri mkoa wa Pwani. Picha na Ayubu Simba

# Pwani Leo

Toleo la Januari 2023|Kazi iendelee

*Imetolewa na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Pwani*


## Pwani Kuendela Kufungua Mtandao wa miundombinu ya Barabara...

**Na Nasra Mondwe**
**Pwani**

Mkuu wa Mkoa wa Pwani Mhe Abubakar Kunenge ameeleza Nia ya Mkoa huo ni kuendelea kufungua mtandao wa miundombinu bora ya barabara inayoakisiana na kasi ya uwekezaji iliyopo Mkoani humo.

Aidha ameeleza, nia ya mafanikio hayo itawezekana endapo kutakuwa na mazingira wezeshi ikiwemo kuondoa migogoro ya wakulima na wafugaji na migogoro ya ardhi.

Akifungua , kikao cha bodi ya barabara Januari 4, 2023, kilichofanyika mjini Kibaha na kuhudhuriwa na wajumbe kutoka katika wilaya mbalimbali za mkoa wa Pwani, Kunenge alieleza kuwa , mtandao wa miundombinu bora unatoa fursa kwa wawekezaji ,kurahisisha usafiri kwa jamii na kufungua mkoa kiuchumi .

Hata hivyo, alisema Mazingira wezeshi yakiimarika na kupunguza migogoro ya ardhi itaisaidia kuinua maendeleo na mkoa kuendelea kuwa kimbilio la wawekezaji.

" Tumechoka migogoro ya wakulima na wafugaji hili ni jambo ambalo kama hatutaliondoa vikwazo vitaendelea kubaki pale pale," Tumeona dhamira ya Rais wetu kufungua mkoa wetu ,hivyo ni wajibu wetu sisi kuangalia barabara zenye tija ,tuangalie mkoa wetu kwa ujumla wake ,tunajua nchi yetu ina vipaombele vingi, lazima tupendekeze miradi yenye hoja ,na inayokubalika yenye kuwagusa wananchi na tija kiuchumi,"

"Tunatakiwa tuwe na hoja inaringanishwa na mikoa mingine, barabara zinasaidia kugusa maisha ya wananchi na kukuza uchumi Lakini ukipata barabara inayogusa wananchi na uchumi inakuwa na tija zaidi "alifafanua Kunenge.


# Pwani Leo

Toleo la Januari 2023|Kazi iendelee

*Imetolewa na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Pwani*





Muonekano wa Daraja jipya la Wami kwa sasa ambapo magari yameruhusiwa kupita. Picha na Ayubu Simba.








Muonekano wa Daraja jipya la Wami kwa sasa ambapo magari yameruhusiwa kupita. Picha na Ayubu Simba.

Pwani Leo
Toleo la Januari 2023|Kazi iendelee
Imetolewa na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Pwani

## RC Kunenge awataka wananchi wa Rufiji kutoa ushirikiano kwa Wawekezaji.

**Na Nasra Mondwe**

**Pwani**

Serikali Mkoani Pwani, imewaasa wananchi wa kata ya Chemchem ,Utete wilayani Rufiji Mkoani Pwani kutoa ushirikiano kwa mwekezaji wa mradi mkubwa wa uzalishaji Sukari Lake Agro sugar estates, unaotarajia kutoa ajira zaidi ya 3,500 na kugharimu dollar za kimarekani milioni 321 ifikapo 2025.

Akitembelea na kukagua eneo la mradi huo leo Desemba 30,2022 Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Mhe Abubakari Kunenge alieleza, kwa upande wa Serikali imembariki mwekezaji huyo kuendelea na mchakato ya uwekezaji kwa manufaa chanya ya kata , wilaya, mkoa na Taifa kijumla.

Alieleza, kiwanda hicho kinakwenda kutatua uhaba wa sukari na kuondokana na uingizaji wa bidhaa hiyo kutoka nje ya nchi.

Aidha Kunenge alieleza ni wajibu wa wazazi na walezi Rufiji Mkoani Pwani kuandaa vijana wao ili waje kunufaika na mradi huu.

"Nimetembelea viwanda 28 kila nilipopita wawekezaji wanatoa changamoto ya vijana wazawa kushindwa kuendelea na kazi ,suala ambalo linasikitisha "alibainisha Kunenge.

Naye Meneja mradi Lake Agro, Abubakar Nassoro alieleza ,wameanza Septemba mwaka 2021, ambapo wapo kwenye hatua ya maandalizi ya vitalu miche ya miwa, wamechimba bwawa la maji linalobeba ujazo wa Lita milioni 4.8,umeme na kuboresha miundombinu mbalimbali.

Alieleza, kiwanda cha sukari kinatarajia kuanza mwaka 2025 kwa kuzalisha tani 300,000 za sukari na pia watatumia kilimo cha mkataba kwa wakulima wa nje.

Pwani Leo
Toleo la Januari 2023|Kazi iendelee
Imetolewa na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Pwani



Mkuu wa mkoa wa Pwani pamoja na kamati ya ulinzi na usalama ya wilaya ya Rufiji alipo tembelea kukagua uwkezaji wa LAKEAGRO wanaotarajia kuzalisha sukari ifikapo 2025. Picha na Ayubu Simba.

Pwani Leo
Toleo la Januari 2023|Kazi iendelee
*Imetolewa na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Pwani*

# Ras Pwani alikabidhi Jukwaa la Uwezeshaji Wananchi Wananqwake kiuchumi kampuni ya Go MAMA yenye mtaji na hisa Bilioni 50

**Na Nasra Mondwe**
**Pwani**

Serikali Mkoani Pwani,imelikabidhi Jukwaa la uwezeshaji wanawake kiuchumi Kampuni Ya GoMAMA yenye mtaji na hisa ya Bilioni 50.

Akitoa rai wakati wa makabidhiano ya majukumu ya Kampuni ya wanawake ya GoMAMA (PLC) kupitia Jukwaa la uwezeshaji wanawake kiuchumi Mkoani Pwani,yaliyofanyika Kibaha , Katibu Tawala mkoa wa Pwani,Zuwena Omari alieleza Jukwaa hilo lihakikishe linahamasisha wanawake kuanzia ngazi ya chini ya Vijiji kujiunga na jukwaa pamoja na vikundi ili waweze kunufaika na fursa mbalimbali zinazopatikana kwa ajili ya kujiinua kiuchumi.

Aidha alilitaka jukwaa hilo kuanzisha majukwaa mapya katika maeneo ambayo bado hayajaundwa sanjali na kubuni miradi ya uzalishaji.

Zuwena alieleza,Ni wakati wa wanawake wa vijiji, vitongoji nao kujiona ni sehemu ya fursa zinazojitokeza kumkomboa mwanamke kiuchumi.

Hata hivyo alieleza kwasasa yapo majukwaa yaliyosajiliwa 945 Mkoani hapo,wajumbe zaidi ya 28,000 ikiwa ni sawa na asilimia 54 .

"Serikali itakuwepo kama ilivyo katika Taasisi nyingine,tutaendelea kuwa washauri kuhakikisha Kampuni inaendelea kung'ara ,sisi Serikali wakati tunashiriki hili suala tulitaka kuona wanawake kwenye vikundi vikiimarika kiuchumi ,nawasihi mkawahamasishe na wenzetu wa chini kujiunga tuone nao wakibadilika kiuchumi na waone ni sehemu ya fursa hizi"

"Kama tumesajili kupata Kampuni hitaji la wanawake kuona wanapiga hatua,asilimia 60 ya umiliki na hisa upo katika majukwaa ya wanawake,hivyo Hawa wenzetu wa hali ya chini tusiwaache nyuma , wanaweza kujiona sio sehemu ya hisa hizi"

Pia Zuwena aliwataka viongozi wa Jukwaa hilo kwenda kutoa elimu ya umuhimu wa Kampuni ya GoMama,Lengo lake ili wanawake wengi waweze kunufaika.

Akishukuru Mwenyekiti wa Jukwaa la Uwekeshaji Kiuchumi Mkoani Pwani,Mariam Ulega "Namshukuru mh.Rais Samia Suluhu Hassan kwani yeye ndio muanzilishi wa majukwaa haya, sisi Kama Jukwaa tunataka tuje na mbinu ya kupiga hatua kwa kwenda na Kasi ya mh Rais kwani tumeona akifanya kazi kubwa ya kuifungua nchi ,na sisi tushapewa dira ,nafasi kwa kukabidhiwa kampunii hii ,Tutahakikisha tunatoa elimu ,tutafanya kazi bila kulala"

"Mimi kama Mwenyekiti nitahakikisha Kampuni inasonga mbele ili kumuunga mkono mh.Rais kuhakikisha mwanamke anainuka kiuchumi"alibainisha Mariam.

Pwani Leo
Toleo la Januari 2023|Kazi iendelee
*Imetolewa na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Pwani*



Katibu Tawala mkoa wa Pwani Zuwena Omari wakushoto pichani akimkabidhi Bi.Mariam Ulega Mwenyekiti wa Jukwaa la Uwezeshaji Pwani cheti cha umiliki wa kampuni ya GOMAMA.Picha na Ayubu Simba.





Pichani ni kushoto ni baadhi ya wawezeshaji wa majukwaa ya uwezeshaji kutoka halmashauri na pichani kulia ni baadhi ya watumishi RS.PWANI.Picha na Ayubu Simba.

Pwani Leo
Toleo la Januari 2023|Kazi iendelee
Imetolewa na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Pwani

# RAS Pwani awataka walimu wasichoke kuelimisha Jamii.

**Na Nasra Mondwe**
**Pwani**

Katibu Tawala Mkoa Pwani Zuwena Omari amewataka walimu wote mkoani Pwani wasichoke kuongea na wanafunzi kuhusu athari za kufeli pia ameeleka wazazi wote wapewe elimu kuhusu umuhimu wa elimu kwa watoto wao.

Hayo ameyasema wakati akifungua kikao kazi cha kuboresha masuala ye elimu kilichowahusisha maofisa elimu Msingi, Sekondari, Waratibu wa elimu kata, Maafisa lishe na udhibiti ubora wa shule kilichofanyi katika ukumbu wa mikutano wa ofisi ya Mkuu wa Mkoa

Zuwena aliwasisitiza walimu kuwa waeendelee kutoa elimu ya malezi kwa watoto na wazazi waendelee kupewa elimu ya kuthamini elimu kwa watoto wao bila kuchoka" mkoa huu una tamaduni zake, kutokana na hilo tuongee na wazazi bila kuchoka hadi watakapobadilika"

Pia ameeleza kuwa, Serikali umejidhatiti kutatua changamoto na kuboresha masuala ya elimu kwa Raslimali watu, fedha na miundombinu.

"Mkoa tumepata madarasa mengine 341 bado maeneo machache ambayo bado hawajamaliza ujenzi wapo kwenye hatua za umaliziaji ,tumeshuhudia mh.Rais dkt Samia Suluhu akijidhatiti kuondoa changamoto hizi za elimu ,wote tumeshuhudia akijenga madarasa mengi na Yale yaliyojengwa kupitia fedha za Uviko ambayo yalisaidia kupunguza msongamano madarasa"alisema Zuwena.

Kuhusu lishe Zuwena alisema kuna tatizo la lishe, suala hilo lihimizwe na elimu itolewe kuhusu lishe kwa manufaa ya watoto na vizazi vijavyo.

Kuhamasisha jamii kuchangia chakula kwa ajili ya wanafunzi ili kupambana na changamoto ya mahudhurio ya wanafunzi shuleni, kuboresha Mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa Halmashauri kuweka kwenye bajeti fedha za ujenzi wa miundombinu.

Aidha ameeleza mkoa utasimamia utekelezaji wa mikakati iliyopangwa ili kuinua kiwango Cha ufaulu na kutatua changamoto zinazokabili sekta hiyo

Akizungumzia taarifa hiyo ya tathmini ya matokeo hayo, katika kikao hicho ,Ofisa elimu Mkoani Pwani Sara Mlaki alieleza ,hali ya ufaulu katika mkoa kwa mwaka 2022 ni asilimia 83.162 ukilinganisha na ufaulu wa mwaka 2021 ambao ulikuwa ni asilimia 84.91 .

Ameeleza kuwa kushuka kwa matokeo hayo imetokana na changamoto ya baadhi ya wazazi kushawishi wanafunzi kufanya vibaya katika mitihani Yao ya kumaliza elimu ya msingi 2022.

Ametaja sababu nyingine kuwa ni baadhi ya walimu kutotimiza majukumu yao katika ufundishaji Kama vile kutokuwa na maazimio ya kazi,maandalio ya somo,nukuu za somo,zana za kufundishia na utoro kazini na udhaifu wa usimamizi na ufuatiliaji kwa baadhi ya maafisa elimu kata hali inayochangia ufundishaji na ujifunzaji kuwa wa kiwango cha chini

Pwani Leo
Toleo la Januari 2023|Kazi iendelee
Imetolewa na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Pwani



1 Zuwena Omari
Katibu Tawala Mkoa wa Pwani



3

Picha namba(3) ni Baadhi ya Maafisa elimu wa Sekondari na Shule za Msingi kutoka halmashauri mbalimbali Mkoa wa Pwani.

Picha namba(4) Katibu Tawala Mkoa wa Pwani Zuwena Omari akimkabidhi mkataba afisa elimu Sekondari Chalinze.Picha na Ayubu Simba.

4





2 Sara Mlaki
Afisa Elimu
Mkoa wa Pwani

# Pwani Leo

Toleo la Januari 2023|Kazi iendelee

*Imetolewa na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Pwani*

## Waandishi wa habari Mkoa wa Pwani wajengewa uwezo utekelezaji mradi wa Shule Bora*

**Na Nasra Mondwe**
**Pwani**

Katibu Tawala wa Mkoa wa Pwani Zuwena Omari amewaasa waandishi wa habari kutumia nguvu ya kalamu zao kuandika taarifa za mradi wa Shule Bora unaolenga kuweka mikakati sahihi na kutafuta suluhisho ili kuhakikisha Watoto wa makundi maalum, wa kike na wa kiume wanapata elimu iliyo kwenye mazingira bora.

Rai hiyo ameitoa leo Disemba 8, 2022 wakati akifungua mafunzo ya uhamasishaji wa mradi wa Shule Bora kwa waandishi wa habari na wasimamizi wa vyombo vya habari mkoani humo ambapo pia aliwaasa kuendelea kuimarisha mahusiano baina ya Serikali na vyombo vya habari ili mradi huo ulete tija.

"Hakuna asiyejua nguvu ya kalamu za waandishi wa habari, kwa kuandika taarifa zinazoaminika kwenye kampeni za maendeleo nchini, sisi Kama mkoa tutaimarisha mahusiano na vyombo vya habari ili kuhakikisha mradi unaleta mafanikio "alifafanua Zuwena.

Akielezea mradi huo, Zuwena alibainisha kuwa umefadhiliwa na mfuko wa UKAI unaolenga kuunga mkono uboreshaji wa elimu msingi Tanzania kwa miaka sita katika Halmashauri 67 mikoa 9 yaTanga, Pwani, Dodoma, Singida, Kigoma, Katavi ,Simiyu, Mara na Rukwa na itahusisha watoto milioni 3.8 katika maeneo hayo ya utekelezaji.

"Utekelezaji wa mradi umelenga kuboresha ufundishaji kwa walimu, kuboresha elimu awali na ya msingi iliyo jumuishi kwa makundi ya watoto wenye mahitaji maalum, kuboresha ujifunzaji kwa wanafunzi pamoja na kuboresha mfumo wa usimamizi wa sekta ya elimu katika kuhakikisha kila kiongozi anawajibika ipasavyo kwa nafasi yake ili kufikia azma iliyokusudiwa" alisema Katibu Tawala huyo.

Kwa upande wake Afisa elimu mkoa wa Pwani Sara Mlaki alieleza kuwa mradi wa Shule Bora ulizinduliwa Kitaifa na Kimataifa mwaka 2021 katika shule ya msingi Mkoani kwenye Halmashauri ya Kibaha Mji mkoani Pwani.

Sara lifafanua kuwa kwa sasa zipo kazi zinazoendelea kufanywa kulingana na matakwa ya mradi ikiwa ni sanjari na uboreshaji wa aufundishaji darasa madarasa ya awali, uimarisha usimamizi wa shule na elimu katika Mamlaka za Serikali za mitaa ambapo wameshaanza kuona matokeo chanya kwani ufaulu umepanda.

Sara alieleza mradi huo unakusudia kuondoa changamoto zinazowakabili watoto kushindwa kusoma, kuandika na kuhesabu, kuondoa tatizo la utoro na kutowapa fursa watoto wenye mahitaji maalumu katika kuendelea na elimu ya sekondari.

Naye Mwenyekiti wa Chama cha Waandishi wa habari Mkoani Pwani, Ally Hengo alishukuru kundi la waandishi kutambuliwa na kushirikishwa kwenye utekelezaji wa mradi huo na akaeleza kuwa wanashukuru waandishi kuachiwa mlango wazi kupata taarifa ama kupewa.

Pwani Leo

Toleo la Januari 2023|Kazi iendelee

*Imetolewa na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Pwani*













1) Katibu Tawala mkoa wa Pwani Zuwena Omari akihutubia kwenye mafunzo yakuwawezesha waandishi wa habari kuhusiana na Shule Bora
2&3) Baadhi ya waandishi wa habari na Maofisa habari wakishiriki mafunzo ya Shule Bora . Picha na Ayubu Simba.

Pwani Leo
Toleo la Januari 2023|Kazi iendelee
Imetolewa na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Pwani

# TASAF yatoa Vifaa vya Usafi kwa Watoto wa Kike Pwani

**Na Nasra Mondwe**
**Pwani**

Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) kwa kushirikiana na Shirika la kusaidia watoto Duniani (UNICEF) umetoa msaada wa vifaa vya usafi 16,754 ambavyo vinatarajia kugawiwa kwa watoto wa kike waliobalehe waliopo kwenye mfuko huo katika Halmashauri Tisa zilizopo mkoani humo.

Vifaa hivyo ni kwa ajili ya usafi ikiwemo sabuni, ndoo pamoja na taulo za kike.

Mratibu wa Tasaf Mkoa wa Pwani,Roselyn Kimaro alieleza lengo ni kufikia watoto hao 16,754 ambapo hadi sasa wameshagawiwa watoto 11,350 na zoezi linaendelea.

Hata hivyo ,aliwataka walengwa hao kutumia vizuri misaada wanayopewa ili kuwasaidia na kuwataka wazazi kuzungumza na watoto wao hasa kipindi wanachobalehe kwa Lengo la kuwa wasafi,kujiepusha na mimba za ututoni na magonjwa ya zinaa.

Roselyn aliwasihi watoto hao kuacha kuchangia taulo zao za kike ili kujiepusha na magonjwa

Nae Mratibu wa Tasaf Chalinze Flora Godfrey Barakana alisema lengo la msaada huo ni kumsaidia mtoto wa kike awe huru hasa katika kipindi cha kupata hedhi yake ya mwezi.

Kwa upande wake Anita Philemon mratibu wa Tasaf Kibaha Mjini alisema vifaa hivyo vitasaidia watoto hao kwa Maendeleo yao shuleni na watapewa mafunzo ya namna ya kutumia kabla ya kuvitumia na kuwaomba taulo za kike ni kwa ajili ya msichana mmoja mmoja na sio vya kuazimana ili kulinda afya zao.

Mnufaika wa Tasaf ,Sadi Athumani alieleza elimu waliyoipata wataenda kuifanyia kazi na kuwa mabalozi kwa wengine kuwafundisha kujenga tabia ya usafi na kujilinda na vishawishi ili kuendelea na masomo kutimiza ndoto yao





Pwani Leo
Toleo la Januari 2023|Kazi iendelee
Imetolewa na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Pwani





Baadhi ya Mabinti Wanufaika wa Mpango wa kunusu kaya Masikini unao Simamiwa na TASSAF pamoja na wazazi wao na Waratibu wa TASSAF walipokabidhiwa vifaa vya usafi. Picha na Ayubu Simba.

Pwani Leo
Toleo la Januari 2023|Kazi iendelee
*Imetolewa na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Pwani*

# Waziri Kairuki amewaagiza viongozi Pwani Kufuatilia ufundishaji wa walimu ili kuongeza kiwanho cha ufaulu na kuboresha elimu

**Na Nasra Mondwe**
**Pwani**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) Angela Kairuki, amewaelekeza viongozi wa mkoa wa Pwani kuweka mkakati wa kufuatilia ufundishaji wa walimu ili kuongeza kiwanho cha ufaulu na kuboresha elimu .

Waziri Kairuki ametoa Maagizo hayo katika kikao kazi cha mapitio ya tathimini ya utekelezaji wa shughuli za uboreshaji na usimamizi wa elimu kwa mwaka 2022 na mpango wa mwaka 2023 kilichofanyika katika viwanja vya Shirika la Elimu Kibaha na kuhudburiwa na maafisa mbalimbali wa elimu kutoka Wilaya zote za Mkoa wa Pwani, Wakurugenzi wa Halmashauri, Maafisa Elimu Kata, Wakuu wa Shule pamoja na viongozi wengine kilikuwa na lengo la kukumbushana namna ya kuboresha elimu ya Msingi na Sekondari.

Amewataka viongozi hao kushughulikia changamoto na kero za walimu ikiwemo kuwalipa stahiki zao pamoja na i fedha za malimbikizo ya mishahara na madeni mbalimbali.

Amesema Serikali ya awamu ya Sita chini ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan imefanya kazi kubwa katika kuboresha mazingira ya ufundishaji kwa walimu na hata kutatua changamoto nyingine.

Amemshukuru Rais Samia kwa jitihada hizo ambazo zimewezesha watoto wengi kupata elimu.
Ametaja jitihasa hizo pamoja na mpango wa elimu bila malipo pamoja na ujenzi wa vyumba vya madarasa ambapo katika kipindi kifupi cha Novemba 2021 hadi Desimba 2022 amejenga madarasa 23000 .

Ameongeza kuwa licha ya kujenga madarasa hayo lakini bado ameendelea kutoa fedha nyingi kwa ajili ya kujenga Shule mpya katika Mikoa mbalimbali hapa nchini zikiwemo Shule za Sekondari za wasichana.

Mbali na kikao hicho waziri Kairuki pia alitembelea na kukagua Shule ya Sekondari ya Sofu iliyopo katika halmashauri ya Mji Kibaha na kufuruhishwa na ujenzi shule hiyo na kuwataka walimu kusimamia vyema miundombinu ya Shule hizo.

Kwa upande wake Mkuu wa Mkoa wa Pwani A b u b a k a r i Kunenge,alisema tayari Mkoa ulishafanya kikao kama hicho na utekelezaji wake umekwenda vizuri.

Kunenge,amesema kuwa walifanya tathmini na kubaini Mkoa wa Pwani Kuna Mila na desturi ambazo zinazorotesha ukuaji wa elimu na tathmini hiyo ilikuwa pamoja na kuwauliza wanafunzi kama Kuna utaratibu wa masomo wanapofika nyumbani wazazi kukagua vitabu na vifaa vingine vya kujisomea.

Pia Kunenge amempongeza Rais wa awamu ya Sita Dkt.Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya hasa katika kutambua masuala mbalimbali ya elimu yaliyopo Mkoani Pwani.

Pwani Leo
Toleo la Januari 2023|Kazi iendelee
*Imetolewa na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Pwani*



Waziriwa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) Angelah Kairuki,alipofanya ziara katika mkoa wa Pwani na kuafanya ukaguzi wa shule mpya za sekondari pamoja na kuzungumza na maafisa elimu na walimu wakuu. Picha na Ayubu Simba.





Pwani Leo
Toleo la Januari 2023|Kazi iendelee
*Imetolewa na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Pwani*

# TANGAZO

KATIBU TAWALA MKOA WA PWANI ANAPENDA KUWAKUMBUSHA WANANCHI WOTE WANAOKUJA KUPATA HUDUMA KATIKA OFISI YA MKUU WA MKOA WA PWANI KUWA HUDUMA ZOTE ZINATOLEWA BURE BILA MALIPO YEYOTE.
HUDUMA HIZO ZITATOLEWA KUANZIA SAA 2:00 ASUBUHI MPAKA SAA 9:30 ALASIRI.
HIVYO WANANCHI WOTE MNATAARIFAIWA KUWA HUDUMA ZOTE ZA SERIKALI NI BURE. NA KAMA ITATOKEA KUNA MALIPO BASI MALIPO HAYO YATAFANYIKA KWA KUPEWA KUMBUKUMBU NAMBA (CONTROL NUMBER) NA SIVINGINEVYO.
KATIBU TAWALA ANAWATADHARISHA WANANCHI WASIKUBALI KUFANYA MALIPO YA AINA YEYOTE YALE KWA KUTUMA FEDHA KWENYE SIMU KWANI WATAKUWA WAMETAPELIWA.
PIA ANAWATAHADHARISHA WANANCHI WOTE ENDAPO WATADAIWA FEDHA KWA AJILI YA KUPATIWA HUDUMA BASI WATOE TAARIFA MARA MOJA KWENYE OFISI ZA UTAWALA ZILIZOPO KATIKA OFISI YA MKUU WA MKOA

MWISHO KABISA ANAWAKUMBUSHA KUWA HUDUMA ZOTE ZA SERIKALI NDANI YA OFISI YA MKUU WA MKOA NI BURE NA HAKUNA MALIPO YA AINA YEYOTE ILE
ASANTE SANA